

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA RUKWA

Telegraphic: "REGCOM"

Simu. No:0252802137/2802138/2802144

Fax No. (025) 2802217/2802318

E-mail:ras.rukwa@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,
P. O. Box 128,
SUMBAWANGA.

10, February, 2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI RUKWA

Katibu Tawala wa Mkoa wa Rukwa Ndg. Tixon Nzunda amewaomba wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kushiriki katika uzinduzi rasmi wa siku ya mazoezi Jumamosi ya arehe 11/02/2017 katika maeneo ambayo yametengwa na Halmashauri katika kila Wilaya.

Ombi hilo limetoka kufuatia maagizo ya Makamu wa Rais Mh. Samia Suluhu aliyoyatoa tarehe 17/12/2016 katika ufunguzi wa kampeni ya kitaifa ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza iliyofanyika katika viwanja vya Leaders Club – Kinondoni.

Katika Kampeni hiyo Mh. Samia Suluhu alielekeza kutengwa siku maalum kwaajili ya wananchi wote kufanya mazoezi ili kuboresha afya za wananchi na kupunguza kasi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa inatarajia kufanya Uzinduzi Rasmi siku ya mazoezi katika uwanja wa Mandela siku ya jumamosi tarehe 11/02/2017, Ofisi inawaomba wale wote watakaopata nafasi ya kujitokeza kwenye mazoezi haya basi makutano ni katika uwanja vya Mandela saa Moja asubuhi, zoezi hili litaongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa Kamishna Mstaafu Zelote Stephen Nzunda alielekeza.

Katika siku hiyo mazoezi mbalimbali yanategemewa kufanyika ikiwemo mazoezi ya viungo, kuvutana kwa Kamba, kufukuza kuku, kukimbia kwenye gunia, mbio fupi na ndefu, netiboli, na mpira wa miguu.

Nzunda aliongeza kuwa kwa kufanya mazoezi tutajenga afya zetu na kuwa na taifa lenye afya bora na hivyo kuongeza uzalishaji na kuchangamsha miili.

Abdulrahman Salim Ally

**Kaimu Afisa Habari
Mkoa wa Rukwa**